

Kule Ndani Ya Kule Ndani

*“Yohana Mt.17:6, “Jina lako nimewadhihirishia watu wale
ulionipa katika ulimwengu;
walikuwa wako ukanipa mimi,
na Neno lako wamelishika”*

Sikiliza kile ambacho Nabii wa Mungu wa wakati huu amesema juu ya hilo:

katika kuzungumzia uzazi wangu wa asili,kuna mambo mengi katika uzazi wangu wa asili ambayo siwezi kujivunia. Mama yangu kwa kuanzia alikuwa ni mwenye dhambi(Zaburi 51:5);Baba yangu alikuwa ni mwenye dhambi. Na walitokea miongoni mwa wapiganaji wa visu na wapiganaji wa bunduki, na wengi wao walikufa na viatu vyao: wanywaji na walevi ,na kila kitu kingine, walitokea Kentuki. Mama yangu alikuwa nusu mhindi na sina chochote cha kujivunia. Siwezi kujivunia mtu wa familia yangu(Warumi 3:10-12).

Lakini utukufu kwa Mungu, kuna kitu kimoja ninachoweza kujisifia nacho, kuzaliwa kwangu kwa pili, ambako kunatoka kwa Yesu Kristo. Naweza kujisifia wazazi hawa tulio nao, kwa maana Yeye ni Baba yangu. Yeye ni Mwokozi wangu. naweza kujisifia yote yale aliyonitendea mimi, kwa sababu sasa nimekuwa mwana wake. Sio mwana tena wa Charles Branham! Mimi ni mwana wa Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Naweza kujisifia kuzaliwa kwangu sasa. Siwezi kamwe kujisifia kuzaliwa kwangu kwa kwanza: Hakuna chochote.....nauonea huo aibu. lakini sioni aibu kule kuzaliwa kwangu kwa pili. Hapana. Hapana. Sionei haya kule kuzaliwa kwangu kwa pili (Yohana 3:1-8;Tito 3:4-7).Amelifanyaje hilo, “kwa kuoshwa kwa maji katika Neno (Waefeso 5:26-27) Hiyo ni sahihi kabisa.

Waaminio wa kweli waliochaguliwa kimbele, wanakaa na Neno, na hawatalipotosha. Haliwezi kupotoshwa, oh! Wana na binti za Mungu, kwa nini hatuwezi kuwa na ushindi huu mkuu ambao tungepaswa kuwa nao wana na binti za Mungu wote? Tunapaswa kuwa nao.Lakini hawatapenda kufanya hivyo hivyo ndivyo tu, kwa sababu sio hasa wana na binti za Mungu kutoka kwenye...

Kile kitu kidogo kule ndani ya kule ndani, hapo ndipo unapoanzia, ambapo ni nafsi yako; halafu kutoka hapo wewe ni roho; halafu unakuwa kiumbe hai. Sasa kiumbe aliye hai anazo hisi tano za kuwasiliana; wa pili anazo hisi tano hizo ni mwili wa nje; kuona, kuonja, kuhisi, kunusa, na kusikia. ule mwili wa ndani una upendo, dhamira, na mawazo, kumbukumbu, na fikira: hisi tano. Lakini kule ndani ya ndani, mtawala/Mwongozaji ni Mungu au Shetani.

Na unaweza kuigiza chochote cha vitu hivi unavyowasiliana navyo.Kama mkristo; au unaweza ukatoa pepo, kama mkristo. lakini kule ndani mtawala wa ule mwanzo, asili yake siyo Mungu. Kamwe haitarudi kwa Mungu. unaelewa hilo? Je Yuda hakutoa pepo?(Matayo10:1-4)Je Kayafa, yule aliyemhukumu Yeye na kumuua, si alitoa unabii? Lakini hakuweza kukaa na Neno. unaona Hiyo ni sawa.

[1] Sasa, hebu niwachoree mduara mdogo. Lakini ninataka ninyi muangalie hapa. Nataka nitengeneze duara moja kwa hili. Nitafanya duara lingine ndani ya duara hili;

hayo ni mawili, halafu sasa nitaenda kufanya duara ndani ya duara hili; hayo ni maduara matatu. Sasa hilo ni wewe. Huyu ni Mungu. Mungu katika utatu ni mmoja na bila ya utatu Yeye siyo Mungu. Hawezi adhihirishwe kwa njia nyingine yoyote .Na hata wewe huwezi dhihirishwa bila kuwa katika hali hizi tatu ambazo uko. Hiyo ni mwili, roho, nafsi,.Bila mojawapo ya hizo, wewe siyo mkamilifu. Unaona? kama ungekuwa huna nafsi, ungekuwa siyo chochote. Kama huna mwili, ungekuwa roho,na siyo mwili. Kwa hiyo Mungu anakamilika katika utatu wa kiumbe; siyo utatu wa viumbe, lakini utatu wa kiumbe kimoja. Baba, Mwana, Na Roho Mtakatifu ni Mungu mmoja wa kweli akidhihirishwa.

Sasa, huyu mtu wa nje ni mwili na nyama, huo ndio tunao uona. Na unawasiliana kwa vitu vitano kwenda kwenye mwili. Na kila aliyekwenda shule ya msingi kama mimi, na atajua kuwa zipo hizo hisi tano zinazoongoza au kutawala mwili; kuona, kuonja, kuhisi, kunusa, kusikia. Bila hizo, huwezi ukaugusa mwili. Hiyo ndiyo njia pekee kuweza kupita kwenye mwili kuona, kuonja, kuhisi, kunusa, kusikia. Unaliona hilo? lionje, lihisi hilo, sasa, huyo ni yule mwovu ambaye yuko nje. Warumi 7:18-21;(Wagalatia 5:16-17).

Sasa, ndani ya huo ni roho, ambayo unakuwa wakati umezaliwa hapa na pumzi ya uhai inapulizwa ndani yako, hiyo roho asili yake ni ya dunia, kwasababu haikutolewa kutoka kwa Mungu, lakini ulipewa, kwa mapenzi ya kuruhusiwa ya Mungu. Sasa unalipata hilo?

Kwa maana kila mtoto anayezaliwa katika dunia, anazaliwa katika dhambi, akiumbika katika uovu (Isaya 64:6) alikuja duniani akisema uongo. (Warumi3:4) Hiyo ni sahihi?

Kwa hiyo yule mtu ndani pale ni mwenye dhambi kwa kuanzia. Lakini sasa anazo hisi tano za kuingilia.....sijui kama naweza zitaja kwa sasa., moja niijuayo ni mawazo, dhamira, upendo, fikira (na kumbukumbu) kuna njia tano za kuwasiliana na roho, huwezi kufikiria kwa moyo wako; inabidi ufikiri kwa roho yako. huwezi kuwa na kufikiri kwa mwili wako wa nje, kwa sababu kufikiri hakuoni, hakuonji, hakunusi, au kusikia. Kufikiria ni kitu ufanyacho akilini mwako. kama umelala au uko nje; mwili wako umelala pale umekufa, lakini roho yako ingefikiri; hapo hisi tano zinazo tawala mtu wa ndani Sasa, kwenda kwa yule mtu wa mwisho ambaye ni nafsi kuna hisi moja tu ambayo inatawala hivyo,na hiyo ni uhuru wa maamuzi, uhuru wa kuamua, kukubali au kukataa.

Na sasa, sababu ya watu leo....sasa, usisahau hili sasa, na utaona ni nini ishara ya Roho Mtakatifu. Unaona? sasa watu wanaweza kuishi hapa kwenye roho, na kucheza katika roho, wanapiga kelele katika roho, wanaenda kanisani katika roho na wanaweza kabisa wakawa na roho wa Mungu akiwapaka mafuta roho zao, lakini bado apotee na bado awe amepagawa tu na shetani kama wawezavyo kuwa katika roho.

“Yeyote atakaye ongeza Neno moja kwenye hili au kuondoa Neno moja kutoka katika hilo.....(Ufunuo22:18-19)Lazima uwe na mkataa mahali fulani. Neno la Mungu ndio mkataa. Chochote kile ambacho lile Neno linasema, hapo sasa hiyo ni sahihi.

Sasa, njia pekee ya kupandia haya maduara kwamba kile uwezachokuwa katika huu utu wa ndani, ni lazima uwe ulijulikana na kukusudiwa kimbele, kwa sababu ulikuwa na Mungu; U sehemu ya Mungu (warumi8:29-30)

Nilikuwa ndani ya baba yangu,nilikuwa ndani ya babu yangu pia na babu yangu. Kwa jinsi ya mbegu.Nilikuwa ndani ya hiyo. Nilikuwa ndani ya Kristo. Ulikuwa ndani ya Kristo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia.(waefeso1:3-4) Alikuwa kukomboa walio wake. Na walio wake ndani yake (Haleluya). Watoto wake ambao walikuwa ndani yake.(Yohana 17:6-8)

Hakuja kukomboa watoto wa shetani(Yohana 17:9) Kamwe hawatalijua hilo. Na ni wenye ufahamu katika njia zao katika kusoma kwao kwa kiakili, kwamba kamwe huwezi ukajilinganisha na wao hata kidogo. Huwezi ukawazidi katika kuzungumza. Lakini kwa Imani unaliona hilo.[2]

Sasa kama, akili zako zinakuambia.....ohhh, hapa upo msumari sasa: kama ufahamu wako wa kiakili unakuambia hili ni kweli, Mungu ni mponyaji wa magonjwa akili zako zinashuhudia kuwa hiyo ni kweli; Lakini kama hakuna mahali pa kulalia Mbegu moyoni mwake, Imani, kuanguka na kulidhihirishe, haiwezi kutokea.

Haijalishi huyu mtu wa nje atajadili vipi na maandiko na kusema ni kweli, hiyo bado hailifanyi kuwa ni kweli.

Mpinga Kristo anajaribu kudanganya hata ingewezekana mteule (Matayo 24:24) haiwezekani kwa sababu haiwezekani; wamechaguliwa. Unaona? vema.

Lakini alisema wale waliopakwa mafuta.....unaona, “Kristo” yamaanisha“wapakwa mafuta”lakini hawa walikuwa wapinzani. walipakwa mafuta, lakini kinyume cha Kristo katika mafundisho yao.Sasa wangeweza kufanya vyovyote vile ambavyo wengine wangepanya.

Sasa kumbuka,uko katika duara ya watatu.Lakini u mtu mmoja.hali tatu za Mungu yule mmoja ofisi za huduma tatu:Ubaba,Uwana,na Roho Mtakatifu na wewe ni mwili, roho na nafsi.

Sasa, mwili wa nje una hisi tano za kukuacha uwasiliane na nyumba yako ya dunia; kuona, kuhisi, kuonja,kunusa na kusikia.Ule wa ndani ambao ni roho, una hisi tano;dhamiri na upendo na kadhalika,lakini ndani ya hiyo,ile nafsi, ina kimoja tu. Hapo ndipo unapoishi.

Roho inaweza kuja nje hapa .na kukupaka mafuta kufanya mambo fulani fulani na unafanya hayo,lakini hiyo haimaanishi umeokoka.Lakini fikiria hilo Kayafa alitabiri (Yohana 18:14). Yuda alitoa pepo. Unaona.Yule Roho alimpaka mafuta.Iko pale mvua hunyesha kwa wema na wabaya; magugu yanaweza kufurahi pamoja na ngano (Matayo 5:43-45).Lakini ni kile ilicho kule ndani ya ndani. Pale ndipo uwezapo. kwa njia ya kiakili unaweza kuikubali na kusema, “oh, kweli, hilo linaonekana zuri, naliadini hilo”Hilo bado halifanyi hivyo.Hapana Bwana na roho anaweza kushuhudia hilo,na bado siyo hivyo.kwa sababu kama ile nafsi haikutoka kwa Mungu, inaweza ikafanya maigizo yote nje hapa,lakini haiwezi kuwa halisi unaweza ukaigiza uponyaji;unaweza ukaigiza kama unao,unaweza ukaigiza kama unaupokea huo.Wakristo wanaweza kuigiza kama ni wakristo,na kuigiza na kuwa wazuri kwenye huo kama iwezekanavyo, lakini hilo halimaanishi umeokolewa.hiyo ni kweli kabisa unaona?Yule roho anaweza akawa pale,roho halisi wa kweli.Roho Mtakatifu anaweza kukupaka mafuta;hilo bado halimaanishi umeokolewa.Ni ile nafsi ya ndani ambayo haiwezi kamwe kufa; ambayo inao uzima wa milele.siku zote ilikuwa uzima wa milele.Unaona? inatoka kwa Mungu:inaenda kwa Mungu;ni ile nafsi.

Sasa,angalia hilo, ni lazima iwe Tano. i-m-a-n-i. nje; roho.Yesu; kule ndani y-a-k-o.unaona? ndio maana ni hisi mama hapa nawaangalia ninyi.siwajui hata mmoja wenu.Roho anaweza kunipaka mafuta,na bado nisimjue hata mmoja wenu.Lakini yule wa ndani ya ndani anapodhihirika, huyo ni Mungu.

Hapo ndipo yule wa nje anapoweza kufikiri.mchukuwe mtu,sema, “vema,unajua,ninajua sipaswi kufanya uzinzi. Lakini,unajua, tena roho ananiambia ninapaswa nisitende uzinzi.Lakini,unaona kule ndani kabisa bado kile kitu kiko pale”.unaona.bado itaongoza hapa, na ni vema uchunge hilo. [3]

Lakini kule ndani kabisa ya mtu yule,kama ile nanga haiko pale,ile mbegu ya Mungu iliyokusudiwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, sijalishi kunatokea nini; hicho kinamshikilia. kiko pale kukaa(Luka8:11). [2]

Lakini kinapoongozwa kutoka ndani,linatupa vyote vilivyo baki hiyo ndiyo iongozayo.Hapo ndipo penye uongozi,kule ndani ya ndani.nafsi inatawala roho inatawala mwili.kwa hiyo kung'ara kwa nje hakufanyi tofauti. wale watu wa kidini nyuma pale(Matayo 23:25-28) ambao Paulo aliwaita “kuta nyeupe”na kadhalika, kwa nje walikuwa waaminio kila namna. na walikuwa na unabii miongoni mwao na kila kitu, lakini kule ndani ya ndani.....kulikuwa na nafsi isiyoyamini (Ezekiel 18:20)

Hiyo ndiyo sababu ninasema watu wanaweza kuruka juu na chini,na kuzungumza kwa lugha;watu wanaweza kupiga makelele,kuweka mikono juu ya wagonjwa,na kuwaponya-na kadhalika kwa imani;mambo hayo yote makuu pale kwa roho, na bado wapotee,wapakwa mafuta..... [3]

Kama unaniadini mimi kuwa nabii wa Mungu,sikiliza maneno yangu.Unaona? Huo ni udanganyifu katika siku ya leo. Je Biblia haikusema kwamba itakuwa karibu sana kiasi cha kumdanganya aliye mteule kama ingewezekana? walioteuliwa ndani kabisa kwenye nafsi.....lakini kama umecheza katika roho,bado unayo mambo ya dunia kuna kasoro.Umezungumza kwa lugha;Paulo alisema, “ninaweza kunena kwa lugha za Malaika na wanadamu, na bado niwe sijaokolewa hata” uh-uh.Aina zote mbili.Unaona? Ninaweza kufanya misisimko yote.Ninaweza kuwa na imani; ninaweza kuhubiri injili;ninaweza kutoa mali zangu kuwapa maskini;ninaweza kulichukuwa Neno katika sehemu za umisionari duniani,na bado niwe bure”(1Kor 13:1-10) Unaona? Ni kule ndani ya ndani.ndugu.Roho yako hugawanyika unapokufa inaruka zake,lakini nafsi yako inaishi. [4]

Na mkristo halisi atakubaliana na yule mtu wa ndani; ile roho iliyokuwa nyuma kule mwanzoni,ambayo ni Neno.kama alivyokuwa ukamilifu wa ninyi wote (kor.2:9:15)ulikuwa ndani yake nyuma pale msalabani (Rumi 6:6).

Alijua kimbele kuwa ungekuwa hapa.Yeye anatangaza tu kile ambacho kingetukia.na ulikuwa ndani yake.Ulikufa pamoja naye.Ulikufa kwa majivuno yako;ulikufa kwa tamaa zako;ulikufa kwa mambo ya dunia.Ulikufa Naye pale kalvari na ulifufuka pamoja naye,pale alipoinuka tena katika siku ya tatu;na kwa sababu umemkubali Yeye, sasa umeketi katika ulimwengu wa kiroho ndani ya Yesu Kristo (Waefeso.2:4-7) Haleluya.Uko hapo. ni yule mtu wa ndani ambaye ataliitika Neno, atashikilia Neno bila kujali.....huwezi kujisaidia.Nimejifunza hilo miaka mingi iliyopita.

Neno la Mungu kamwe haliwezi kushindwa.Litashinda bila kujali ni nini.Ndipo nikajua kuna kitu kule ndani kishindacho kufikiri kote,kitu fulani ndani ya misisimko yote. Kila kitu kama hicho. kulikuwa na mtu wa ndani aliyeshikilia katika saa ile; hakuna chochote kingeweza kufanya hivyo.kila fikira, kila kiwezacho kuonyeshwa, kila kitu kingeweza kithibitisha kuwa siyo sawa, nami nilikuwa niko makosani, lakini Neno la Mungu ambalo lilikusudiwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia lilishikilia kule ndani.

Ndugu, dada, ngoja nikuambie; hicho ndicho kitu pekee,usijaribu kufikiria hilo.usijaribu kuwa na nywele ndefu kwa sababu nimesema hivyo.Usijaribu kufanya hitu hivi kwa sababu tu katika mwili.....usijaribu tu kulifanya ili kukubaliana.Lakini ukae mbele za Mungu mpaka kitu fulani kule ndani.....

Wengi wenu wanafikiri, kwa sababu una nywele ndefu,inamaanisha utaenda mbinguni.Hiyo haimaanishi hivyo.Wengi wao hufikiri,kwa sababu ni mwanamke mwadilifu, utaenda.....haimaanishi hivyo.Wengi wao hufikiri,kwa sababu kanisa lao na liko kwenye hili na kundi hili kubwa na madaktari wakuu wa theologia.Hilo halimaanishi hivyo.unaona?wengi wanafikiri kwa sababu wanazungumza kwa lugha, wana Roho Mtakatifu, Hilo halimaanishi hivyo.ingawa Roho Mtakatifu anazungumza kwa lugha.Lakini mpaka kile kitu halisi cha kweli,Roho Mtakatifu pale atakubaliana na kila Neno.....

Kama Roho Mtakatifu ndani yako atakufanya unene kwa lugha anaangalia nyuma pale na (Roho mtakatifu)halikubaliani na Neno lililobakia lote,hapo sasa hiyo ni roho isiyo sahihi.inabidi ije kutoka ndani,ambayo ni Neno tangu mwanzo,Hapo mwanzo wa kuumba kwa Mungu hapo Mungu alipoanza kuumba na kukuleta katika hali ya kuishi.....(Mwanzo 1:26-27).Unaona ulianza nyuma pale kama mbegu na ikatenda na kuendelea mpaka ulipo sasa,Na sasa ninyi wote mlikuwa ndani ya Kristo.(Waefeso1:3-4).Halafu Kristo alipokufa .Alikuwa kuwakomboa ninyi wote.Na wewe ni sehemu ya hili Neno.Na itakuwaje Biblia yote hiyoItawezekanaje katika dunia, wewe ulikuwa sehemu ya Neno,usikubaliane na sehemu ile iliyobakia au sehemu yoyote ile.

Oh ndugu yangu ,dada,sasa kila mmoja wenu awe na ufahamu ninajua hiyo inamaanisha nini.unaona? angalieni tu kaa karibu na Kristo.ngoja niwaonye ninyi kama wahudumu wa injili usichukuwe ujinga wowote.Usiwaze chochote, kaa pale mpaka yule wa ndani ya ndani amewekewa nanga katika Neno, kwamba uko hasa ndani ya Kristo kwa sababu hicho ndicho kitu pekee ambacho kitaenda.....kwa sababu tuko katika wakati wa udanganyifu sana ambao tumewahi kuishi, ndani yake.Ungemdanganya hata aliye mteule kama ingewezekana, kwa sababu wana upako.Wanaweza wakafanya chochote ambacho wengine wanafanya.

Safisheni maisha yenu.Lipeni madeni yenu; msidaiwe na mtu.Yesu alisema,Sasa,Sasa simaanishi kitu kama kodi ya nyumba na vitu kama hivyo unapaswa uwenavyo.Ondoa vitu vyote mkononi mwako.Fanya kila kitu kiwe sahihi.kuwa tayari.kumbuka ni katika jina la Bwana kitu fulani kitaenda kutokea.
[2]

Nukuu za kiingereza:

[1]Nguvu ya kubadilisha (65-1031m) Aya 307-312

[2]Nawe hujui (65-0815) uk 14/17-18/19/23/24/28/36

[3]Matendo ni imani iliyodhihirishwa (65-1126)Aya 201-211

[4]Uongozi (65-1207)Aya 316-319

jiwe la kiroho la kujengea na 171 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa: Charles E. Y. Kanju,

Box 5138, Tanga

E-mail: chaelika@hotmail.com

Cell.phone 0784704299